# Serikali yaja na mwarobaini kuharakisha kesi mahakamani

**Na Anastazia Anyimike, Dodoma**

SERIKALI imezindua mfumo wa kielektroniki wa usimamizi wa kesi (CMIS) uliounganisha taasisi zote za haki jinai ili kuziharakisha.

Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora, George Simbachawene alisema hayo jijini Dodoma jana.

Waziri Simbachawene alisema hayo wakati wa uzinduzi wa mfumo huo uliotengenezwa na Mamlaka ya Serikali Mtandao (eGA) kwa kushirikiana na Ofisi ya Taifa ya Mashtaka.

Simbachawene alisema mfumo huo umekamilika katika wakati sahihi ambao Rais Samia Suluhu Hassan anaendelea na jitihada za kuimarisha utoaji haki kwa wananchi.

Alisema mfumo huo umeunganishwa na mfumo mkuu wa serikali wa kuwezesha mifumo kubadilishana taarifa (GovESB).

Simbachawene alisema mfumo huo umeanza kubadilishana taarifa na mifumo ya baadhi ya taasisi za hakijinai kama vile Polisi, Taasisi za Kuzuia na Kupambana na Rushwa (Takukuru) na Mahakama.



Alisema hadi sasa kesi za jinai 17,411 zimesajiliwa kwenye mfumo huo na kati ya hizo, 7,361 zimefika mwisho na kutolewa hukumu na 10,050 zipo hatua za uamuzi.

Alihimiza taasisi nyingine za umma ambazo bado zina kiwango kidogo cha utekelezaji wa jitihada za serikali mtandao kuongeza matumizi ya tehama ili kuongeza ufanisi na kuboresha utoaji huduma kwa wananchi.

Naibu Waziri wa Katiba na Sheria, Pauline Gekul alisema wizara hiyo imejizatiti kuimarisha jitihada za kuhakikisha inatengeneza mifumo madhubuti ya Tehama ili kutoa huduma bora kwa wananchi.

"Haki ni suala muhimu sana na inapaswa kutolewa kwa wakati kwani haki iliyocheleweshwa ni sawa na haki iliyonyimwa, hivyo kupitia mifumo ya Tehama tunataka kuhakikisha haki zote zinatolewa kwa wakati," alisema Gekul.

Awali, Mkurugenzi wa Mashitaka, Sylvester Mwakitalu alisema mfumo huo utatunza kumbukumbu zote ikiwamo hati za mashitaka na hukumu na utakuwa na uwezo wa kuonesha jalada lipo kwa wakili gani na limechukua muda gani.

Mkurugenzi Mkuu wa eGA, Benedict Ndomba alisema kuzinduliwa kwa mfumo huo ni utekelezaji wa dhamira ya serikali ya kuboresha mifumo ya utendaji kazi.

"Tulipotoka ni historia, kwa sasa DPP anaweza kufanya ufuatiliaji wa kesi kwenye wilaya na mikoa, lengo ni kuhudumia wadau wetu kwa ufanisi, huu mfumo mzuri twendeni kubadilika ili mifumo ilete tija," alisema Ndomba.

# Samia apongezw… wa umoja, usala…

**Na Zena Chande**

RAIS Samia Suluhu Hassan amepongezwa kwa kutoa kauli iliyotoa msimamo wake kuhusu umoja, usalama na amani ya nchi.

Jumatatu wiki hii Rais Samia alisema hakuna mwenye ubavu au misuli ya kuligawa, kuliuza taifa hili au kuharibu amani na umoja nchini.

Alisema hayo Arusha wakati wa maadhimisho ya miaka 60 ya Kanisa la Kiinjili la Kilutheri Tanzania (KKKT) yaliyofanyika katika Chuo Kikuu cha Tumaini Makumira.

Mwanasiasa mkongwe na Mwenyekiti mstaafu wa Baraza la Vyama vya Siasa Tanzania, John Shibuda alisema kauli ya Rais Samia imewathibitishia Watanzania nchi ni salama.

"Amethibitisha yeye ni kiongozi mvumilivu na anatambua anaongoza watu wa matabaka mbalimbali," alisema Shibuda ambaye ni mwanachama wa chama cha siasa cha ADA-Tadea.

Alisema mfumo wa uongozi wa Rais Samia ni kama mwalimu anayefundisha wanafunzi wenye vipaji maalumu na wasio na vipaji hivyo jukumu lake ni kuhakikisha wote wanafika pamoja wanapokwenda.

Shibuda alisema mfumo wa uongozi wa Rais Samia ni wa kulinda amani na kukuza uchumi kama ilivyokuwa kwa waasisi wa taifa.

"Tanzania tuache wivu na nongwa dhidi ya watu wabunifu sababu kila awamu inapoingia madarakani ina ubunifu wake kama kuna hitilafu mahali njia pekee ni kukosoa kwa staha na sio kupiga makelele," alisema.

Katibu Mkuu Msaidizi wa Chama cha Wananchi (CUF) Tanzania Bara, Magdalena Sakaya alisema kauli ya Rais Samia inaweza kusaidia kuondoa mpasuko ulioanza kujitokeza.

"Kauli ya Rais ni kama imetoka kwa mtu anayejua kinachoendelea…kwamba yanayofanywa tunajua na tuko imara hakuna wa kutugawa," alisema Sakaya.

Aliongeza: "Nilitegemea nisikie mapema kutoka kwake

# Watoto wa Tabora … kutenganishwa Sau…

**Na Matem Kayera**

MADAKTARI watakaofanyia upasuaji watoto Watanzania kuwatenganisha nchini Saudi Arabia wamesema wana imani watafanikiwa.

Watoto hao pacha ambao ni Hassan na Hussein wenye umri wa mwaka mmoja na miezi 11 walisafirishwa jana kwenda nchini Saudi Arabia kwa ndege binafsi iliyotumwa na Serikali ya Saudi Arabia.

Ndege hiyo iliwasili saa saba mchana na kuondoka saa nane kamili jana katika Kiwanja cha Ndege cha Kimataifa cha Julius Nyerere (JNIA).

Daktari Bingwa wa Upasuaji na Watoto wa Hospitali ya Taifa Muhimbili, Zaitun Bohary ambaye amewasindikiza watoto hao akifuatana na muuguzi, Alfreda Kapinga alisema watoto hao walipokelewa katika Hospitali ya Taifa Muhimbili wakiwa na wiki mbili.

Pacha hao walizaliwa wakiwa wameungana sehemu ya kifua, tumbo na nyonga.

Dk Bokhary alisema pacha hao wanahitaji jopo la madaktari wa nyanja mbalimbali ili kuwatenganisha.

"Timu ya madaktari inayohitajika ni kubwa ambayo sisi kwetu kwenye Hospitali ya Taifa ya Muhimbili hatuna timu kubwa ya kiasi hicho ya kuweza kufanya upasuaji mkubwa kama huo japokuwa tuna uwezo wa kufanya upasuaji lakini tunahitaji timu kubwa zaidi ya kufanya upasuaji," alisema.

Aliongeza: "Saudi Arabia wana uzoefu wa zaidi ya miaka 40 wanafanya upasuaji kama huu katika Hospitali ya Mfalme Abdullah, mpaka sasa wameshafanya upasuaji wa aina hizi takribani wagonjwa 130 walioteganishwa."

Mmoja wa madaktari waliokuja na ndege hiyo ambaye hakutaka jina lake liandi…